SHEIKH MUHAMMAD BÂZMÛL

HAKURIDHIKA NA TABIA YA NDUGUYE MDOGO AHMAD

http://www.kulalsalafiyeen.com/vb/showthread.php?t=1261

Mfasiri: Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad

Ndugu ‘Ali Abu Haniyyah (*hafidhahullâh*) amesema:

Kutokamana na ninayoyajua kutoka kwa *fadhilat ash-Sheikh*, Muhammad Bâzmûl, ni kwamba ni mtu mwenye fahamu njema, muadilifu na mwenye vipimo vya usawa. Ni mtu mwenye ‘ilmu pana, kalamu isiyo kifani na manhaj iliyosalimika. Na daima alikuwa akiwaheshimu, kuwakirimu na kuwafadhilisha Mashayekh kadiri ya daraja zao, nasi twamuhesabu kuwa kama hivyo na wala hatumtukuzi mbele ya Allâh; Kwahivyo, nilimpigia simu siku ya Jumatatu, 16th Muharram, 1430 Hj, siku inayolingana na tarehe 12th January, 2009, ili atuangaziye juu ya mambo yanayoendelea kwenye jukwaa la *ma-Salafi* ili apate kuweka mipaka kwa ndugu yake (Dr. Ahmad Bâzmûl) na kejeli zake dhidi ya Sheikh wetu ‘Ali (Hasan).

Ninayoyajua mimi kihakika ni kwamba, sheikh hakuridhika na tabia za ndugu yake, Ahmad. Sheikh (Muhammad Bâzmûl) alitoa sifa nyingi kwa sheikh wetu, ‘Ali na alikuwa na unyenyekevu sana, twamuombea Allâh ampe ziyada katika wema na fadhla, akasema (*hafidhahullâh*):

“Mimi nina heshima na taththmini kubwa kwa muheshimiwa Sheikh ‘Ali na Mashayekh wa Jordan, bali mimi nawazingatia kuwa Mashayekh hao (wa Jordan) wana fadhla kubwa miongoni mwa vijana wa *ki-Salafi* wa katika milki za kiarabu na ulimwengu mzima kwa ujumla. Tumefaidika vya kutosha kutokana na vitabu vyao, mimi binafsi akiwemo Sheikh ‘Ali na Sheikh Salîm wakiwa katika daraja ya waliokuwa miongoni mwa Mashekhe zangu. Mimi siwezi kujiingiza nikajifanya niko kwenye daraja zao pamoja nao, na wala sijiweki nafsi yangu mbele kuwa katika daraja ya kuzungumza kuwahusu wao au kuwa sawa na wao.”

Vilevile [Sheikh Muhammad Bâzmûl] amenieleza yakwamba bado yeye hajakichunguza kitabu kipya [cha Sheikh ‘Ali] *Manhaj Salaf us-Swâlih* na alizungumza kwa njia ya *ki-‘ilmu* kulihusu suala hilo, likiwa ni miongoni mwa *ikhtilafu* zisizolazimu *tashnî’* (ukosoaji wa matusi) wa mwengine aliye na rai tafauti katika mas’ala ya *Ijtihâd*. Vilevile aliniambia yakwamba yeye amemnaswihi ndugu yake (Ahmad) asijiingize kwenye *fitan* miongoni mwa Mashayekh na awaachie mas’ala kama hayo Wanavyuoni wakubwa. Kwahivyo, mimi [Abu Haniyyah], nilipomwambia yakwamba ndugu yake [Ahmad Bâzmûl] amejiunga na kuingia kwenye mabishano haya kwa kuandika, yeye [Sheikh Muhammad Bâzmûl] akanitakia mimi kheri na niendelee kutoa naswiha. Kisha [Sheikh Muhammad Bâzmûl (*hafidhahullâh*)] akasema maneno yafuatayo:

“Mimi naona yakwamba katika mas’ala haya, pindi mas’ala ya ikhtilafu miongoni mwa Mashayekh yanapochipuka, basi wanafunzi wa ki-‘ilmu kama mfano wangu mimi na walio chini kuliko mimi wasijiingize, na wawaachie wanavyuoni wenyewe. Ama kuhusu ndugu yangu Ahmad, basi nilizungumza naye na nikamwambia: ‘Ewe Sheikh Ahmad, usijiingize kwenye mas’ala haya.’ Akanijibu: ‘Mimi sijamwita Sheikh ‘Ali jina lake, sijamtaja na wala kitabu chake, lakini hatahivyo mimi nimezungumzia kuhusu utafiti na fikra kama Madda.’ Wallâhi, haya ndiyo yaliyokuwa maneno yake. “Mimi bado sijauchunguza utafiti wenyewe”, na akasema yakwamba kuna mambo aliyo na matatizo nayo ambayo Sheikh ‘Ali aliyoyafungamanisha kuhusiana na: Mas’ala ya kumsusiya mtu wa bid’ah na suala la kupambana na mtu wa bid’ah linalohusiana na Manhaj ya Salafi. Mimi nikamwambia Sheikh Ahmad: ‘Ewe Sheikh Ahmad, wawachie *kalâm* hii wanavyuoni wakubwa! Wewe hufai kujiingiza kwenye mas’ala haya’. Na akanitakia mimi kheri. Kwahivyo, mpaka sasa, na Wallâhi mpaka saa hii nnapozungumza na wewe, mimi sijakichunguza kitabu cha Sheikh ‘Ali.

“Ndani ya nafsi yangu, mimi bado nimeshikilia msimamo wa rai yakwamba wanafunzi wa ki-‘ilmu kama mfano wangu, au walio chini yangu, hawafai kuchimba sana kwenye *kalâm* za Mashayekh miongoni mwao kuhusiana na mas’ala haya. Kwahivyo wachana na Mashayekh wayajadili mas’ala mpaka haki iweze kubainishwa kwa wote ili yule mwenye neno la kusema lenye dalili na ushahidi adhihirike.”

Hii ni kwa ajili ya kutumia mfumo ufuatao ambao ni kuwa: ‘Ikhtilafu ya rai zetu haifai kuharibu mapenzi’. Ni nani ambaye hapa katika ardhi hii asiyepinga chochote? Ni nani asiyekuwa na rai tafauti na wengine? Nani? Salafiyyah haimaanishi yakwamba *Ijtihâd* zetu au rai zetu katika kila suala litakuwa ni hilohilo moja? Hii si maana ya Salafiyyah. Lakini hatahivyo, ndugu husema hivyo kuhusiana na mas’ala uliyotutajia wewe [ndugu ‘Ali Abu Haniyyah] na kubuni msingi kutoka katika Usûl wa Salaf us-Swâlih. Mas’ala kama hayo yanahitaji Subira na kunyamaziwa, na shabâb hawafai kuhusika katika matatizo haya. Insha-Allâh mimi nitaendelea katika kutoa naswiha zangu na kuwa na matumaini yakwamba Allâh atatuja’aliya kufuzu, twatumai Allâh atatuja’aliya kufuzu... Miongoni mwetu sisi, *kalâm* hazifai kuwa *Shadîd* na kuwa ni makali, hususan kama mfano wa Ahmad, mimi mwenyewe au Sheikh ‘Ali. Wallâhi, mimi sionelei yakwamba mwanafunzi aishushe adabu yake, *Allâhul Musta’ân,* mimi nafuatilia jambo nililo na uwezo nalo, *Walâ hawla walâ Quwwata illâ billâh.”*

Hawa *ma-Ghulât*, tayari wameshajaribu kuweka *tafsîl* yao wenyewe yenye kugeuza kuhusu maneno ya Sheikh Muhammad Bâzmûl hapa:

http://albaidha.net/vb/showthread.php?t=13717

tumekiweka hiki kiungo chao cha mtandao kwa min-ajil ya kuwaonyesha ndugu jinsi hoja zao zilivyo dhaifu katika miangaza iliyonaswihiwa na Shaikh Muhammad Bâzmûl!